JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

S. L.P 123,
Simu: (023) 2334013,
Nukushi: (023) 2333726
Barua pepe: rbcmtwara@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz

MTWARA MEI, 2023

USHIRIKIANO KATI YA TAKUKURU MTWARA NA WADAU WALETA TIJA MIRADI YA MWENGE

Katika kipindi cha **Januari – Machi 2023,** TAKUKURU Mkoa wa Mtwara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, huku mkazo ukiwekwa katika UZUIAJI RUSHWA hasa kwenya miradi ya maendeleo pamoja na elimu ya kuhamasisha wananchi washiriki kikamilifu kwa kuwajibikaji na kuchukua hatua stahiki ili kuzuia rushwa, kwakuwa jukumu la kuzuia rushwa ni la kila mmoja wetu kwa nafasi yake.

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023 zilizinduliwa katika mkoa wa Mtwara ambapo kwa mkoa wa Mtwara miradi yote 54 yenye thamani ya billion 31 iliridhiwa. Mafanikio haya yanatokana na Mpango mahususi na shirikishi wa uelimishaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo uliotekelezwa na TAKUKURU Mkoa wa Mtwara kwa kuelimisha wahusika wa miradi katika halmashauri zote tisa za mkoa wa Mtwara na kwa pamoja kuitembelea miradi yote iliyopangwa kutembelewa na Mbio za mwenge wa uhuru mwaka 2023.

Aidha ushauri ulitolewa mapema kabisa juu ya kuziba mianya ya rushwa na kutekeleza miradi kwa uadilifu. Ushirikiano wa dhati kutoka kwa Mh. Mkuu wa Mkoa na ofisi yake ambayo kimsingi ndiyo waliongoza shughuli hizi kwa kuweka mipango na mikakati ya utekelezaji kupitia vikao vya pamoja na kuunda timu za ukaguzi zilizopita halmashauri zote na kukagua, kushauri na kusaidia pale palipohitaji usaidizi. Timu za ukaguzi zilizoundwa na ofisi ya mkuu wa mkoa zilihusisha wajumbe kutoka TAKUKURU mkoa wa Mtwara.

Wah. Wakuu wa Wilaya nao kwa nafasi zao walisimamia vyema utekelezaji wa miradi hii kwa kuhakikisha thamani yafedha inapatikana

na taratibu zote zinafuatwa. Wah . madiwani, Wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa idara na kamati zilizohusika kwenye miradi walishiriki kila mmoja kwa nafasi yake kwa lengo la kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa ubora na kwa wakati. Wananchi walihusishwa vyema katika miradi kwa kiwango cha kuchangia nguvu zao ili kufanikisha miradi hii kwa maendeleo yao.

Ushirikiano huu umetupa kuoana dhana halisi ya kila mmoja wetu kubeba jukumu la kuzuia rushwa kwa kutimiza wajibu wake. Kwa kufanya hivyo Mafanikio ya Mkoa wa Mtwara ni yetu wote.

Ninatoa wito kwa wadau wote kuwa ushirikiano huu uendelee katika miradi yote kwani miradi yote inapaswa kutekelezwa kwa uadilifu ili thamani ya fedha ipatikane na wananchi wapate huduma stahiki.

1. UZUIAJI RUSHWA:

TAKUKURU Mkoa wa Mtwara **imefuatilia utekelezaji wa miradi thelathini na mbili (32)** yenye thamani ya zaidi ya **shilingi bilioni 6** (6,274,388,439.07) katika sekta za Miundombinu, Elimu, Afya na Maji. Hii inajumuisha miradi iliyotembelewa na mbio za Mwenge wa Uhuru Mwaka 2023. **Miradi 11** iliyofuatiliwa ilionekana na mapungufu kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini:-

S/N	JINA LA MRADI NA THAMANI	YALIYOBAINIKA	HATUA ZILIZOCHUKULIWA
	MTWARA		
1	Mradi wa matengenezo ya barabara wenye zabuni namba, AE/092/2022-2023/MT/W/15 Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani. (67,735,600/=)	Baadhi ya kazi kukosa ubora wake wakati wa utekelezaji wake. (workmanship) mfano viraka na mifereji kutomaliziwa vizuri katika sehemu chache.	Kuwashauri wasimamizi wa miradi husika kuhakikisha kasoro zilizo onekana/bainika zinarekebishwa.
2	Mradi wa matengenezo ya barabara wenye zabuni namba AE/092/2022-	Baadhi ya kazi kukosa ubora wake wakati wa utekelezaji wake. (workmanship) mfano	

	2023/MT/W/20 unaosimamiwa na TARURA – Wilaya katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani.(128,245,000/=)	viraka na mifereji kutomaliziwa vizuri katika sehemu chache..	
3	Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Shangani (60,000,000/=)	Kulikuwa na mapungufu katika umaliziaji milango,rangi, vigae.	
4	Ujenzi wa Bweni la Wanafunzi wenye mahitaji maalum Nanguruwe katika Shule ya Msingi. (100,000,000/=)	Mteremko kwenye eneo la kupanda watu wenye mahitaji maalum (ramp) lilikuwa na mteremko mkali	
5	Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mkomo katika Halmashauri ya Mji Nanyamba. (81,000,000/=)	Ubora hafifu wa kazi hasa kwenye upakaji rangi.	
6	Mradi wa asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya vijana, wanawake na wenye ulemavu katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. (101,893,396/=)	Marejesho kutofanyika kama ilivyopangwa.	Madeni yafuatiliwe kwa umakini zaidi na ili wadaiwa warejeshe kwa wakati.
7	Mradi wa asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya vijana, wanawake na wenye ulemavu katika Halmashauri ya Mji ya Nanyamba. (77,907,150/=)		Muda wa urejeshaji uangalie uhalisia wa mkopo husika.

8	Mradi wa ujenzi wa barabara kiwango cha lami barabara ya Nanguruwe – Namayakata – Mkunwa yenye urefu wa kilometa 1.7 katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara. (949,139,000/=)	Kulikuwa na shida kwenye mifereji.	Kuwashauri wasimamizi wa miradi husika kuhakikisha kasoro zilizo onekana/bainika zinarekebishwa.
NANYUMBU			
9	Ujenzi wa vyumba vya madarasa viwili katika Shule ya Sekondari Mikangaule. (40,000,000/=)	Kulikuwa na nyufa kwenye baadhi za kuta.	Walishauriwa kurekebisha.
TANDAHIMBA			
10	Ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika Shule ya Sekondari Tandahimba. (80,000,000/=)	Baadhi ya milango haikuwa na ubora.	
NEWALA			
11	Mradi wa ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa ndani (IPD) katika kituo cha afya Mkunya (100,000,000/=)	Baadhi ya kazi hazikufuata vipimo kama ilivyoanishwa kwenye BOQ mfano ukubwa wa uwazi wa madirisha. Pia upungufu katika ubora wa kazi za rangi	Walishauriwa kurekebisha.

CHAMBUZI ZA MFUMO

S/N	CHAMBUZI ZA MFUMO	LENGO	YALIYOBAINIKA	MAKUBALIANO
1.	Uchambuzi wa mfumo wa	Kutathmini mfumo wa	Hakuna maeneo maalum ya Halmashauri	

	uendeshaji wa masoko katika Wilaya ya **Nanyumbu**.	utambuzi wa wafanyabiashara katika masoko. Kuchunguza mfumo wa usimamizi wa mapato yatokanayo na tozo. Ushuru katika masoko na kiwango cha mapato kinachopokelewa na Halmashauri kwa mwezi. Kuchunguza mfumo wa usimamizi wa matumizi yatokanayo na ada na ushuru.	lililotengwa kwa ajili ya kuendesha shughuli za masoko ya biashara inapelekea watu binafsi kutoa maeneo yao na kuendesha shughuli za kukusanya mapato katika masoko hayo na kusababisha Halmashauri kukosa mapato. Halmashauri haikusanyi ushuru kwenye soko lililopo ambalo eneo lake linalomilikiwa na mtu binafsi katika Kijiji cha kilimahewa. Hivyo Halmashauri haipati mapato kutokana na biashara inayofanyika eneo la soko. Kamati zinazosmamia soko hili hazina usimamizi wa afisa biashara wala afisa yeyote wa serikalini hivyo zinapokusanya fedha za ulinzi na usafi hakuna rekodi sahihi ya makusanyo ya utunzaji wa fedha zilizokusanywa kwa kila mwezi na malipo matumizi	

			yake kwa kila mwezi. Hivyo fedha hizo ni rahisi kutumika kwa matumizi binafsi. Kutokana na soko kuendeshwa kwenye eneo la mtu binafsi uwezekano wa kutozwa gharama kubwa za kupangisha ardhi hiyo ikilinganishwa na tozo ambazo zingetozwa na Halmashauri hivyo hali hiyo inafifisha mwamko wa wananchi kufanya biashara katika soko hilo. Hali hiyo inasababisha baadhi ya bidhaa kuuzwa maeneo yasiyo rasmi ili kukwepa kulipa gharama hizo.	
2	Warsha kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko katika Wilaya ya Nanyumbu.	Kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko na kuweka maazimio ya namna ya kuboresha		Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu itenge eneo kwa ajili ya shughuli za soko. Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu itoe elimu kwa wafanyabiashara ili waweze kuona umuhimu wa kuhamia eneo la serikali

				lililotengwa kwaajili ya shughuli za soko. Halmashauri ya Wilaya Nanyumbu isimamie shughuli zote za usafi wa soko lililopo sasa kwa lengo la kuthibiti uchafu katika soko hilo.
3	Warsha kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani.	Kujadili matokeo ya uchambuzi wa mfumo wa uendeshaji wa masoko na kuweka maazimio ya namna ya kuboresha		Ufuatiliaji wa kibali cha kutumia Silaha ndani ya Soko Kuu kwenye Mamlaka husika ili ulinzi uimarishwe katika soko hilo. Utunzaji wa taarifa mzuri wa kuzingatia wafanya biashara wakudumu Pamoja na wale muda mfupi na wanao ingia na kutoka ili kuwepo na kumbuku nzuri za taarifa kuhusiana na wafanya biashara sokoni. Maombi kupelekwa katika Ofisi za Manispaa kuhusiana na kuongezewa

				miundombinu ya vyoo katika Soko Kuu ili kupata wepesi katika huduma hiyo. Ufuatiliaji wa karibu kwa wanaochelewa kulipa ad ana ushuru kwa wakati ikiwa ni Pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria kwa ambao hawataki kulitekeleza hilo. Maombi kwa Mkurugenzi wa Manispaa kuhusiana na vyombo vya usafiri vinavyotoka Wilayani kufika Stendi Kuu/Stendi ya zamani ili kuchochea shughuli za kibiashara Sokoni hapo kwani kwa sasa zinaishia Stendi mpya, Mkanaledi.
4	Tathmini ya Hatari ya Rushwa katika usimamizi wa Mazao ya	Kutathimin uwezekano kutokea vitendo vya Rushwa katika maeneo yaliyoainishwa		

	Misitu.	Kutathimin madhara vitendo vya rushwa katika maeneo yaliyoainishwa.		

2. UELIMISHAJI UMMA:

Kazi za Uelimishaji Umma zilizofanyika ni zifuatazo:-

NA	KAZI	UFAFANUZI
1	Kutembelea na kuimarisha klabu za wapinga Rushwa katika shule za msingi na Sekondari na vyuo	klabu za wapinga Rushwa 45 zilizopo katika shule za msingi na sekondari pamoja na vyuo ziliimarishwa kwa kupewa elimu ya kukuza uzalendo na uadilifu.
2	Kufanya maonesho mawili.	Katika maonesho haya Elimu ilitolewa ambapo Wananchi walikumbushwa juu ya jukumu la kuzuia Rushwa na namna wanavyoweza kushirikiana na TAKUKURU katika kuzula Rushwa na wananchi pia walipata fursa ya kutoa maoni yao juu ya namna ya kuboresha ushirikiano ili kudhibiti vitendo vya rushwa.
3	Mikutano ya hadhara vijijini ili kuwafikia wananchi wengi walioko pembezoni.	Ilifanyika mikutano ya hadhara 16 ambapo wananchi walihimizwa kushiriki na kusimamia miradi ya maendeleo ili kuzuia rushwa na zaidi kuhudhuria mikutano ya vijiji ilikutoa michango yao na kuhoji mapato na matumizi ya kijiji pale ambapo wanaona kuna shida.
4	Semina watumishi wa umma makazini na kutoa elimu juu ya rushwa mahala pa kazi.	Semina 20 zilitolewa kwa lengo la kuwakumbusha watumishi kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni, aratibu na miongozo iliyopo na kujiepusha na vitendo vya Rushwa.

5	Utoaji wa habari na mkala.	Makala 5 na taarifa kwa umma 1 zilitolewa ili kufahamisha umma juu ya mambo mbalimbali yanayofanyika katika uzuiaji rushwa pamoja na kuhabarisha umma juu ya utendaji wa TAKUKURU (M) Mtwara.

Vilevile elimu ya rushwa ilitolewa kwa wateja wanaotembelea ofisi zetu na kutaka ushauri na machapisho mbalimbali kwa ajili ya rejea.

3. TAKUKURU RAFIKI

TAKUKURU Mkoa wa Mtwara kwa ushirikiano na wadau imetekeleza program ya TAKUKURU RAFIKI katika kata 8. Kero 48 Zilibainika na hatua zilochukuliwa ni kama zilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini:-

Na.	Sekta	Kero Zilizotambuliwa	Hatua zilizochukuliwa
1	Maji	9	Kero nyingi zilitatuliwa kwa wajumbe katika kikao kupewa uelewa sahihi wa kero husika na kuelewa. Kwa yale yaliyohitaji ushiriki wa watoa huduma TAKUKURU inaendelea kuwasiliana nao ili kufanya kikao na watoa huduma na badae wananchi katika kata husika kuelezwa matokeo.
2	Nishati	6	
3	Afya	8	
4	Elimu	6	
5	Ardhi	8	
6	Maendeleo ya jamii	9	
7	Miundombinu	2	

Programu hii imewezesha kubaini udhaifu mkubwa wa wananchi kutohudhuria mikutano ya kisheria ya mitaa na vijiji ambapo kero nyingi zinazosababishwa na kutokuwa na maelezo na uelewa sahihi zingetatuliwa. Aidha, mikutano huwa ni jukwaa sahihi la wananchi kutoa mawazo yao katika utatuzi wa kero.

4. UCHUNGUZI NA MASHTAKA:

Pamoja na kuhamasisha sana suala la **KUZUIA RUSHWA,** bado wapo ambao hufanya TAKUKURU ilazimike kufanya kazi za mapambano dhidi ya Rushwa. Katika kipindi husika, tumepokea **malalamiko 55,** ambapo **taarifa za rushwa zilikuwa 27** na **zisizo za rushwa ni 28.**
Taarifa 27 zinazohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo:

Na	Sekta	Idadi	Hatua zilizochukuliwa
1	Elimu	4	Uchunguzi unaendelea ili kubaini ukweli wa tuuma hizi.
2	Afya	3	
3	Utawala	3	
4	TRA	3	
5	Ushirika	3	
5	Ardhi	2	
6	Uchukuzi	2	
7	Kilimo	2	
8	mahakama	1	
9	Polisi	1	
10	Redcross	1	
11.	RITA	1	
12.	Nida	1	

Taarifa 28 zisizohusu rushwa zilihusu sekta au maeneo yafuatayo:

Na	Sekta	Idadi	Hatua zilizochukuliwa
1	Sheria	3	Walalamikaji walishauriwa na tatizo kubwa ni ukosefu wa taarifa sahihi na kutojua ofisi halisi ya kushughulikia tatizo husika.
2	Mahakama	2	
3	Utawala	2	
4	Elimu	1	
5	Ujenzl	1	
6	Baraza la kata	1	
7	Dini	1	
8	Ardhi	1	
9	Elimu	1	
10	TASAF	1	
11	Benki	1	
12	NIC	1	
13	Fedha	1	
14	Hifadhi jamii	1	
15	Mawasiliano	1	
16	Nishati	1	
17	Binafsi	8	

5. MASHTAKA

Katika kipindi tajwa takwimu za kesl ni kama zilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:-

Wilaya	Kesi Mpya Zilizofunguliwa (2)	Kesi Zilizotolewa Maamuzi	Kesi Zinazoendelea Mahakamani(14)
Mtwara	1		3
Masasi			4
Newala	1		4
Tandahimba			2
Nanyumbu			1

6. MIKAKATI YA APRILI– JUNI 2023:

TAKUKURU Mkoa wa Mtwara, inatarajia katika robo ya Aprili-Juni, 2023, kuimarisha juhudi za kuzuia rushwa kwa kukagua miradi ya maendeleo na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika vita dhidi ya rushwa kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji ikiwemo vipindi vya redio pamoja na uelimishaji katika mikusanyiko mbalimbali.

Pia tutaendelea kufuatilia makusanyo na matumizi ya fedha za umma na kuchukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma. Aidha, tutafanya warsha na wadau kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika ili kuweka maazimio ya namna bora ya kuziba mianya ya ufujaji iliyobainishwa.

7. HITIMISHO:

Mwisho, tunawashukuru wananchi wa Mkoa wa Mtwara kwa kutuunga mkono katika vita hii yetu sote. Tunawasihi wengine wote wenye mtazamo kwamba hii ni kazi ya Serikali pekee waachane na fikra hizo batili na wajiunge nasi ili kuongeza nguvu katika jeshi la wazalendo, waadilifu na wanaojisikia fahari kuzuia rushwa. Umoja ni nguvu.

"Kuzuia rushwa ni jukumu lako na langu, tutimize wajibu wetu".

Imetolewa

ENOCK P. NGAILO
MKUU WA TAKUKURU (M) MTWARA
0738150156